

# Wananchi waomba silaha Msumbiji

Mzalendo  
8/11/87

p. 2

Na Mwandishi Wetu

**WANANCHI** wa Msumbiji wanaoishi katika Bonde la Chitima, wamemuomba Rais Joaquim Chissano awapatie mafunzo ya kijeshi na silaha ili waisaidie Serikali katika juhudi zake za kuwatokomeza magaidi wa nchi hiyo wanaoungwa mkono kwa hali na mali na utawala wa kibaguzi wa Afrika Kusini.

Akizungumza na wananchi hao, Ndugu Chissano alisema kwamba amekwenda katika sehemu hiyo ili kupata kauli yao kama wanataka kuongozwa na Serikali yake au wanataka kuongozwa na magaidi hao ambao wamekuwa wakiwaua wananchi.

Kiongozi huyo wa Msumbiji aliwaambia wazi wazi wananchi hao kwamba wana uhuru wa kuchagua nani awaongoze na kuwahakikishia kwamba hawatakamatwawala kuchukuliwa hatua kama watachagua kuongozwa na magaidi.

Kwa kauli moja wananchi hao walimhakikishia Rais Chissano kwamba wanataka kuongozwa na Serikali yake na kutokana na kauli hiyo aliwashauri kuandaa kuunda vikundi vya ulinzi dhidi ya mashambulizi ya magaidi.

Wakati huo huo, mabalazi wa nchi za nje walioko mjini Maputo wiki hii walitembelea eneo la Tanninga ambako kujitokea mauaji ya watu 278 yaliyofanywa na magaidi.

Akikagua mabaki ya mabasi

yaliyochomwa moto. Balozi wa Marekani, Bibi Melissa Wells, aliwaambia waandishi wa habari waliofika katika eneo hilo kwamba, "Sioni gari lolote la kijeshi hapa. Kwa nini ilikuwa ni lazima kufanya uharibifu kama huu."

Bibi Wells ambaye awasili mjini Maputo mwezi uliopita kuanza kazi



yake hiyo aliyaeleza mauaji hayo kuwa ni ugaidi na ujahili na kwamba atapeleka taarifa moja kwa moja mjini Washington ili kueleza Serikali yake kile alichokiona.

**Katika hatua nyingine ya harakati za**

ukombozi, majeshi ya Chama cha Ukombozi wa Namibia (SWAPO) yamewaua askari 11 wa Makaburu na kuwajeruhi wengine katika jimbo la Ovambo, Kaskazini mwa Namibia.

Utawala wa Makaburu umekiri katika taarifa yake ya kijeshi kwamba ulipata kipigo hicho wakati askari wake walipojaribu kuvamia askari wa SWAPO.

Utawala wa kibaguzi wa Wazungu wachache wa Afrika Kusini wiki hii baada ya kuona kwamba unalemewa na harakati za wazalendo, umeamua kumuachia huru mmoja wa viongozi wa wazalendo, Ndugu Govan Mbeki, ambaye alikuwa akitumikia kifungo cha maisha kwa miaka 23 iliyopita.

Ndugu Mbeki, 77, alihukumwa pamoja na kiongozi wa chama cha ANC, Ndugu Nelson Mandela kifungo mwaka 1964 kwa kile kilichodaiwa kuwa walifanya njama za kuuangusha utawala wa Makaburu kwa nguvu.

Taarifa iliyotolewa na Makaburu ilisema kwamba Ndugu Mbeki aliachiwa pamoja na wafungwa wanne wengine wa kisiasa ambao walikuwa wakitumikia kifungo cha miaka 20. Wengine walioachiwa ni Ndugu J. Nkosi, Ndugu M. Matsobone, Ndugu W.S. Tshikila na Ndugu V.T. Masuka.

Nchini Uganda, ambako majeshi ya Serikali ambayo yalikuwa yakipambana na majeshi ya kile kinachojitua kikundi cha kidini, imeweka amani mayozuia kuhubiri dini hadharani mpaka kuwe na kibali.

Taarifa ya polisi iliyotangazwa na Redio Uganda ilisema kwamba wata wote wanaotaka kuhubiri dini nje ya makanisa au misikiti au katika viwanja vya mikutano watalazimika kwanza kupata vivali kutoka polisi na mipango ya uangalizi wa polisi itatanywa.

Polisi imechukua hatua hiyo kutokana na migongano mingi ya kidini iliyojitokeza mwaka huu kwa sababu ya kuhubiri dini hadharani.

Huko Kenya watu wapatao 24 waliumia na wengine 100 kutiwa mbaroni na polisi mjini Mombasa, baada ya kutokea mapambano kati ya wasilam wapatao 4,000 na polisi waliokuwa wakiamandama kupinga hatua ya serikali ya kuondoa idhini iliyotolewa ya kuhubiri dini.

Kapteni Blaise Compaore ambaye alinyakua madaraka nchini Burkina Faso, alijitangaza kuwa kiongozi wa nchi na Serikali na kuhadhiisha baraza la mawaziri.

Kutokana na kujinyakulia madaraka, Compaore alimuua kiongozi wa nchi huyo, Kapteni Thomas Sankara na watu wengine 100 kitendo ambacho kimeantwaa na wapenda haki duniani.